

# KUIPITIA UPYA FATWA YA LAJNA DHIDI YA SHEIKH ‘ALI HASAN AL- HALABI.

## FATWA YAJIBIWA NA SHEIKH ‘ALI HASAN AL-HALABI

الحجة القائمة في نصرة اللجنة الدائمة

---

[Bofya kiungo hiki ujipatie Nakala ya Hujjatul Qaimah.](#)

Muhammad Awadh Basawad,  
[www.qssea.net](http://www.qssea.net)

Mnamo mwaka wa 1421 H, ambao ni sawiya na mwaka wa 2000 CE, Kamati ya Kudumu (Lajna ad-Dâ’imah) walitoa fatwa dhidi ya vitabu viwili vilivyotungwa au kuandikwa na Sheikh ‘Ali Hasan al-Halabi. Kitabu kimoja, kwa jina la [“Tahdhîr min Fitnati-t Takfîr”](#), na kitabu chengine , kwa jina la [“Saihatu nadhir”](#). Fatwa yenyewe ilikuwa ni ya kumlaumu muandishi wa vitabu hivyo viwili kwa kulingania kwenye ‘aqîdah ya murji’ah. Vilevile Fatwa hiyo ikambandikiza lawama muandishi kwa kusambaza kwa njia ya kuwazulia urongo Ibn Kathîr na Sheikhul Islâm Ibn Taymiyyah. Fatwa yenyewe imejaa kasoro nyingi ambazo wanavyuoni walio viongozi wakubwa walitoa maoni yao wakati huo wa fatwa hiyo.

Amesema Sheikh Ibn Uthaymîn kuihusu fatwa hiyo, “Fatwa hii ni ya makosa kutoka kwa Lajna, hata mimi nilishangazwa na fatwa hii. Waislamu kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu wameisoma fatwa hii, mpaka wengine pia wamenipigia mimi simu kutoka Marekani (USA) na Uropa (Europe). Hakuna aliyefaidika na fatwa hii isipokuwa ma-Takfiri (wenye kukufurisha watu) na watu wa hamasa za mapinduzi.” (Uk. 25).

Vilevile akasema, “Sikuridhika mimi kwa kutolewa fatwa hii kwa sababu ndani yake muna mambo yatakayosababisha vurugu kwa watu. Naswiha yangu kwa wanafunzi wa ki-ilmu ni kwamba waipuuze fatwa ya fulani au fulani.” (Uk. 29).

Sheikh ‘Abdulmuhsin aliulizwa kuhusu “athari ya fatwa juu ya yule ambaye iliyotolewa kwa ajili yake”. Akajibu Sheikh: “Haina athari yoyote juu yake, hata chembe.” [*yaani; haina madhara yoyote juu yake, haimuathiri kivyovyote, haimzuii chochote*] (Uk. 29).

Utaratibu:

Amesema Sheikh ‘Ali Hasan, “Nilimtembelea, muheshimiwa mwenye fadhla, Sheikh Sâlih bin Fawzân al-Fawzân - Allâh amuhifadhi - nyumbani kwake, Makkah katika masiku ya Mina, kwenye msimu wa Hajj ya mwaka wa 1421 H (sawiya na mwaka wa 2000). Nilikuwa nimefuatana na baadhi ya Mashayekh pamoja na wanafunzi wa ‘ilmu, nikamuuliza, “Hiki kitabu changu **“Tahdhîr min Fitnati-t Takfîr”** kilifanyiwa utafiti na kukaguliwa na Kamati ya Kudumu (Lajna) wenyewe? Walikisoma kitabu hicho wao wenyewe? Kufuatilia kutoka kwenye (suali) hilo, fatwa ilitolewa kwa muafaka wao na sahihi zao zote?

Au kwani ulikuwa uchunguzi huu (kwenye vitabu vyangu) wametayarishiwa na kuletewa Kamati ya Kudumu (Lajna) na mtafiti maalum, au msaidizi au muhudumu? Ni muundo gani wa utaratibu uliotumika?

Basi muheshimiwa mwenye fadhla, Sheikh Sâlih bin Fawzân al-Fawzân - Allâh amuhifadhi - akajibu, “Kwa hakika, wao, Kamati ya Kudumu (Lajna) hawakuvisoma vitabu vyote wao wenyewe. Waliletewa utafiti ukiwa umetayarishwa, kisha baadae nao wakaandika ukosoaji wao juu yake (huo utafiti) lakini sisi tunaurejesha nyuma utafiti huo kwenye Usûl (*yaani; kitabu*) Uk. 7

Kuna idadi ya vipengee vilivyogunduliwa wakati wa kutolewa fatwa hiyo na yaliyomo kwenye fatwa yenyewe. Miongoni mwa vipengee hivyo ni:

1. Fatwa imebeba madai yakwamba Sheikh ‘Ali Hasan analingania imani yakwamba vitendo si sharuti kwa kusihhi Imani. Suala hili halikujadiliwa au halikutajwa kwenye vitabu viwili vilivyokosolewa. Uk. 42.
2. Fatwa imebeba madai yakwamba, muandishi wa vitabu hivyo viwili ameiwekea kufr kikomo kwenye sampuli mbili za Ukafiri Mkubwa. Juhûd na Takdhîb, na kwamba Ukafiri Mkubwa unaweza kutokea tu kwa kuhalalisha yaliyo haramu, haliyakuwa ukweli wa mambo ni kwamba Muandishi wa vitabu hivyo (Sheikh ‘Ali Hasan al-Halabi) ameeleza waziwazi katika mojawapo ya vitabu hivyo vilivyokosolewa na Kamati ya Kudumu. Ameeleza katika **“Saihatu nadhir”**, Uk. 47 yakwamba Ukafiri Mkubwa umegawanyika kwenye sehemu tano (Uk. 59).

**TANABAH!** Jambo la kejeli katika mas’ala haya ni kwamba baadhi ya wale waliokuwa kwenye mstari wa mbele katika kumtetea Sheikh ‘Ali Hasan al-Halabi dhidi ya tuhuma za Irjâ’ dhidi yake wakati huo uliopita, waliyafasiri na kuyachapisha majibu yake kwa Kamati ya Kudumu, tangu mwaka wa 2000 - yanayopatikana [hapa](#), sasa hivi wamegeuka kichwa chini miguu juu, na sasa hivi wanadai yakwamba Sheikh ‘Ali Hasan al-Halabi amekuwa Murji’. Na mfano wa hayo unapatikana [hapa!!!](#)